**MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE (MB) KWENYE MKUTANO NA WAANDISHI WA HABARI KATIKA UKUMBI WA IDARA YA HABARI MAELEZO JIJINI DODOMA TAREHE 30 JANUARI 2026**

**Kazi na Utu ..!**

***Ndugu Wanahabari*;** Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuwezesha kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Pia, napenda niwapongeze na kuwashukuru kwa utayari wenu wa kushirikiana na Ofisi hii katika kuwaelimisha na kuwafikishia wananchi taarifa muhimu zinazohusu masuala ya utumishi na utawala bora ili umma wa Watanzania uweze kuhabarishwa. Ninawashukuru sana kwa mchango wenu huu mkubwa kwa ustawi wa Taifa.

***Ndugu Wanahabari;*** Lengo la Mkutano wa leo ni kupeana taarifa juu ya utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jumhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa tarehe 28 Agosti, 2025 katika ufunguzi wa Kampeni za Uchaguzi kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM).

***Ndugu Waandishi wa Habari;*** Kimsingi, jukumu kuu la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maeneo mbalimbali

ikiwemo Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma kuanzia upatikanaji wake, Uendelezaji wake, Utawala wa Utumishi wa Umma, Uwajibikaji/Mikataba ya Utendaji wake, Malipo ya Mishahara, Maadili/Uadilifu wake na Maboresho katika Utumishi wa Umma.

***Ndugu Wanahabari;*** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye pia alikuwa mgombea wa nafasi ya Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi, alitoa ahadi mbalimbali ambapo kwa upande wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora aliahidi ndani ya siku 100 baada ya kuchaguliwa kwake atafanya mambo makubwa katika maeneo mawili kama ifuatavyo; mosi, kutoa ajira 12,000 katika mgawanyiko nitakaoueleza punde. Pili, kuanzisha mfumo wa uwajibikaji ambapo viongozi wataongea na wananchi moja kwa moja kwa njia ya mtandao, katika kutekeleza hilo yafuatayo yalifanyika. Mhe Rais alitoa kibali cha nafasi 12,000 za ajira zikiwemo nafasi 5,000 za kada za Afya na nafasi 7,000 za Walimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati.

***Ndugu Wanahabari;*** Maelekezo haya ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutangaza ajira hizo yanatokana na malengo ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya Mwaka 2025 ambayo imetambua eneo la fursa za ajira kwa vijana na iliyojitokeza katika Ibara ya 49: CCM inatambua

umuhimu wa kuimarisha Utumishi wa Umma kama mhimili muhimu wa kutekeleza misingi ya demokrasia na utawala bora.

***Ndugu Wanahabari;*** nikiwa ndiye Waziri mwenye dhamana ya kusimamia Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba sasa mniruhusu nitoe mrejesho kwa Watanzania kuhusu utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais katika eneo la utumishi wa umma na utawala bora kama ifuatavyo;

Katika utekelezaji wa ahadi ya kutoa kibali cha ajira kwa nafasi 12,000, (walimu 7,000 na watumishi wa Afya 5000) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitekeleza agizo hilo kama ifuatavyo; baada ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kuapishwa tarehe 3 Novemba, 2025 kibali cha Ajira ya watumishi 12,000 kilitolewa. Kwa kuzingatia kifungu cha 32 (7) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, sura ya 298 jukumu la kuendesha mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma linafanywa na Sekretarieti ya Ajira, hivyo Sekretarieti ya Ajira ilitoa tangazo la ajira.

Baada ya kupokea maombi, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (PSRS) iliratibu usaili ambao ulifanyika katika Mikoa yote Tanzania na vituo mahsusi kwa Unguja na Pemba. Tarehe 13 – 14 Disemba, 2025 Usaili wa mchujo (aptitude test) ulifanyika kidijitali na matokeo ya usaili huo

yalitolewa siku hiyo hiyo ambayo usaili ulifanyika. Tarehe 15 – 23 Disemba, 2025 ulifanyika usaili wa mahojiano kwa waombaji wote waliofaulu usaili wa mchujo.

***Ndugu Wanahabari****;* Kuanzia tarehe 11 hadi tarehe 20 Januari, 2026 Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imewapangia vituo wasailiwa wote ambao walifaulu usaili. Barua za kuwapangia vituo wasailiwa waliofaulu zilitumwa moja kwa moja kwenye akaunti za waombaji badala ya barua hizo kufuatwa Makao Makuu ya Sekretarieti ya Ajira Dodoma. Mpaka sasa jumla ya watumishi **8,416** kati yao, watumishi wa kada ya elimu ni **3,694** na watumishi wa kada ya Afya ni **4,722** wameripoti katika Halmashauri mbalimbali na watumishi **735** ambao waliripoti kabla ya kufunga orodha ya mshahara wameingizwa kwenye payroll ya Serikali na tayari wamekwishapata mshahara wa mwezi Januari 2026. Kati ya hao watumishi 956 wa elimu na 305 wa afya wapo kwenye mchakato. Aidha, watumishi wote wataingia kwenye orodha ya mshahara wa Serikali (Payroll) kwa kadri wanavyoripoti katika vituo vyao vya kazi.

***Ndugu Wanahabari;*** Baada ya zoezi la ajira kukamilika nataka nitoe angalizo kwa waajiriwa wapya kuwa wanapaswa kuripoti ndani ya siku 14 tangu kupokea kwa barua zao za kupangiwa kituo cha kazi na watakaokiuka kuripoti ndani ya muda

uliopangwa nafasi zao zitachukuliwa na wasailiwa wengine ambao wapo katika kanzi data. Pia napenda kutoa maelekezo kwa waajiri kuwa, baada ya kuwapokea watumishi wa ajira mpya wanapaswa kuwasilisha taarifa zao za ajira kwa Mhariri Mkuu wa Gazeti la Serikali ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili ziweze kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

**Ndugu Wanahabari,** Vilevile, kumekuwa na maombi mengi ya kubadilisha vituo vya kazi, nitoe rai kuwa hakutakuwa na mabadiliko ya vituo vya kazi kwakuwa nafasi hizi za ajira zimetolewa kulingana na uhitaji wa kila Halmashauri au mwajiri husika. Hivyo, kubadili kituo maana yake ni kupunguza idadi ya watumishi waliopangwa kwenda Halmashauri husika. Ili kutoathiri ugawaji wa nafasi hizi, hakuna mabadiliko yoyote ya vituo yatakayofanyika.

***Ndugu Wanahabari;*** Serikali itaendelea kutoa nafasi ya ajira na kuzitangaza, hivyo tunawaomba vijana wote wenye sifa waendelee kuomba nafasi mbalimbali kwa kadri zitakapotangazwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

***Ndugu Wanahabari;*** Pamoja na hilo la Ajira 12,000 kama nilivyoeleza Mheshimiwa Rais pia alielekeza kuanzisha mifumo

rafiki ya uwajibikaji ambapo Viongozi wa Kitaifa, Sekretarieti za Mikoa, Wilaya na Watendaji wengine wa Serikali watoe taarifa na kujibu maswali kutoka kwa Wananchi kwa njia ya Kidigitali na ujumbe mfupi wa simu za mkononi (SMS) bure.

***Ndugu Wanahabari;*** Katika kutekeleza hili, Ofisi ya Rais, Menejiementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeboresha Mfumo wa e-Mrejesho. Mfumo huu wa kielektroniki wa kutuma, kupokea na kushughulikia taarifa za malalamiko, Mapendekezo, Maulizo, Maoni na Pongezi zinazotolewa na Wananchi kuhusu huduma zinazotolewa na Serikali ulianzishwa mwaka 2022 na kuunganishwa katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zote nchini. Kufuatia maelekezo ya Mhe Rais, maboresho ya kuongeza Dirisha la ‘’Sema na Kiongozi’’ katika mfumo huu lilianzishwa.

Lengo la Mfumo ni kuimarisha Utawala Bora unaosimamia uwajibikaji na usikivu wa watumishi wa Umma kwa Wananchi. Aidha, utekelezaji wake unasimamiwa na Mwongozo wa Ushughulikiaji wa Mrejesho wa Wananchi kuhusu Huduma zinazotolewa na Serikali wa mwaka 2023.

Katika ngazi ya Taifa, Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Manaibu wao hutumia dashibodi ya pamoja ya

wizara kufuatilia na kutoa maelekezo kuhusu malalamiko yote yanayohusu wizara zao. Ngazi ya Mkoa inawahusisha Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa na kwa ngazi ya Wilaya, inawahusisha Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tawala wa Wilaya. Viongozi katika ngazi zote wana dashibodi zinazowapa taarifa na takwimu mbalimbali za malalamiko yaliyopokelewa na wanaweza kupitia taarifa, kutoa maoni, kutoa maelekezo na kufuatilia hatua zinazochukuliwa hadi suala kufungwa kabisa.

***Ndugu wanahabari,*** Wananchi wanaweza kuwasilisha maoni au malalamiko kupitia tovuti ya e-Mrejesho au Programu ya Simu (Mobile App) au USSD (*152*00#) kwa kuchagua **Sema na Kiongozi**, kisha kuchagua ngazi ya uongozi wanayolenga. Baada ya kuwasilishwa, sekretarieti husika hupokea taarifa, huku viongozi wakipata fursa ya kutoa maelekezo, kuacha maoni na kufuatilia utekelezaji wa hatua hadi shauri lifungwe, hivyo kuhakikisha sauti za wananchi zinasikilizwa na kushughulikiwa ipasavyo.

Mfumo huu unaratibiwa na Waziri, Katibu Mkuu (U), Katibu Mkuu (Ikulu) na viongozi wa ngazi za juu akiwemo Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, na wanatazama matokeo. Dirisha hilo limekamilika na hatua za kuwawezesha watumiaji wa mfumo zinaendelea.

***Ndugu wanahabari,*** Aidha pamoja na mambo ambayo nimeyaeleza hapo juu yapo mambo ambayo Ofisi ya Rais Menejimenti ya utumishi wa Umma imeyafanya ikiwa ni maagizo ya Mhe Rais. ***Mosi,*** Ofisi ilizingatia maelekezo ya Mhe. Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa tarehe 18 Novemba, 2025 wakati wa uapisho wa Mawaziri na Naibu Mawaziri kuhusu kufanyika kwa Semina Elekezi ya Mawaziri kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa.

Katika kutekeleza agizo hilo, ORMUUB kwa kushirikiana na OR- IKULU iliendesha mafunzo ya Semina Elekezi kwa Mawaziri na Manaibu Waziri walioteuliwa Novemba, 2025. Semina Elekezi iliyoongoozwa na kauli mbiu ***"Nafasi na Wajibu wa Mawaziri katika Utumishi wa Umma na Kufikiwa kwa Dira 2050 na Malengo ya Ilani ya Uchaguzi 2025"*** ilifanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 1- 4 Disemba, 2025, ambapo jumla ya Mawaziri 27 na Naibu Mawaziri 29 walihudhuria. Mafunzo hayo yalilenga kuimarisha uwezo wa Viongozi hao kiutendaji.

***Pili**,* Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia taasisi yake ya **'Watumishi Housing Investment – WHI'** katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa umma, imekamilisha ujenzi wa nyumba **54** za makazi kwa watumishi wa umma zilizojengwa katika Halmashauri za Wilaya 5 katika maeneo magumu kufikika hapa nchini kupitia **Mradi wa Makazi ya Watumishi wa Umma Wilayani Awamu ya I** (District Public

Servant Housing Scheme Phase I). Ujenzi wa nyumba hizo umegharimu kiasi cha Shilingi 3.19 Bilioni ikiwa ni awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huo. Aidha, nyumba 15 kati ya zilizokamilika ujenzi wake ni kwa ajili ya watumishi wa Sekta ya Afya na nyumba 39 kwa ajili ya Sekta ya Elimu (Shule za Msingi na Sekondari). Vilevile katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia taasisi ya Watumishi Housing Investment kwa mwaka wa fedha 2025/26 imetenga kiasi cha Shilingi 4.27 Bilioni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 78 kwa ajili ya makazi ya watumishi wa umma katika maeneo magumu kufikika. Nyumba 33 kati ya hizo ni kwa ajili ya watumishi wa Sekta ya Afya na Nyumba 45 kwa ajili ya Sekta ya Elimu.

***Tatu,*** ninapenda kuwajulisha kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ameridhia kibali cha Ajira ya Watumishi 41,500 za watumishi wa Kada mbalimbali kama vile watumishi wa Kada za Afya, Walimu, Kilimo, Afya, Uvuvi, Wahandisi, Zimamoto na Uokoaji, Uhamiaji, Magereza, Jeshi la Polisi na watumishi wa kada mbalimbali. Hivyo, naendelea kutoa rai kwa Watanzania wenye sifa kuendelea kujitokeza kwa wingi kuomba ajira katika Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma watapotangaza nafasi mbalimbali za ajira.

***Ndugu Wanahabari;*** Kwa kuhitimisha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa maelekezo yake ya kuhakikisha wananchi hasa vijana

wanapata ajira na kunufaika na huduma mbalimbali zinazotolewa na Serikali anayoiongoza. Sisi wasaidizi wake tunaahidi kumsaidia kwa dhati katika kutekeleza maelekezo anayoyatoa ili wananchi waweze kupata huduma bora.

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**

**KAZI NA UTU........**

*Mungu Ibariki Afrika!*

*Mungu Ibariki Tanzania!*